Jiwe la kiroho la kujengea No.114

# UONGOZI WA MUNGU.

*Warumi 8:14- kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. (Wagalatia 5:18). Lakini mkiongozwa na Roho, hampo chini ya sheria.*

Sikiliza kile Nabii wa Mungu asemacho juu ya hilo.

Huna budi kuchagua kiongozi wako chagua leo unachagua uzima au kifo Chaguo lako litaamua kikomo chako cha milele, unachochagua.kumbuka Yesu alisema, "Unifuate". (Luka 18:18-22). Umealikwa usiku wa leo kufanya hivyo. Na kumfuata hata kwenye uzima wa milele huna budi kukubaliana na masharti yake, hiyo ni kweli, Neno. Sijuu ya kanuni za Imani, si kulingana na maoni ya watu, si kulingana na yale mtu yeyote anawazia, bali aliyosema Mungu kulihusu.

Kumbukeni, Yesu alisema, "unifuate. Ondolea mbali uliyo nayo. Ukanifuate". Na hiyo ndio njia pekee ya kupata uzima wa milele. Hilo ndilo shauri pekee alilompa mtu huyu. Ndilo shauri pekee alilompa Mfanyabiashara huyu. Ndio shauri pekee ambalo mtu yeyote. Chaguo lake, yeye anafanya uwamuzi wake. Maamuzi yake ni makamilifu kila mara. Nasi hatuna budi kumfuata, ndio njia pekee ya kupata uzima wa milele. Kwa hiyo uongozi wa Mungu ni: fuata Neno lililothibitishwa la wakati huu na Roho Mtakatifu.

Hatuna budi kufuata kila siku, kila saa ya siku, kila hatua ya njia, hatuna budi kuongozwa na Bwana Yesu Kristo. Kama hatuongozwi, tunachukuwa uongozi wa maisha ya kidhehebu. Na maisha ambayo hayamfuati Kristo kila siku hayastahili.
Unapozaliwa kwa roho, unakuwa kiumbe kipya, na kasha Mungu anaanza kushughulika nanyi kama wana na mnaongozwa kwa Roho wa Mungu.

Paulo alokuwa Mkristo halisi. Hakuwa akifanya tamshi lolote lisilo sahihi, alikuwa amefundishwa na Roho Mtakatifu tena kusubiri juu ya Neno. Sasa alikuwa amefundishwa njia moja (na Gamalieli). Lakini Mungu amemfundisha njia nyingine sasa. Alikuwa amefundishwa na Roho mtakatifu kumsubiri bwana (Isaya 40:31). Haijalishi vile matamanio yake yalikuwaje. Ona alijua kumsubiri Bwana. Na hapo ndipo watu wengi leo wanaleta shutuma juu ya Neno. Walitoka wakiwa na shauku. Ni mikutano mingapi ya uamsho imeachwa chini kwa sababu ya kitu kama hicho, kwa sababu wainjilisti hawasubiri waone kile Bwana atakachosema! Lakini Paulo alimsubiri tu Roho Mtakatifu amwambie kipi chakufanya. Popote Roho alipo mwongoza…..

Hiyo ndio sababu na …..Wahuduma wengine wanakuja na kuniuliza (kuomba) kwenda katika sehemu zao, nasubiri mpaka nijiskie kuongozwa kwenda. Kasha kama nikija, ninakuja tuu katika jina langu mwenyewe (kama mkija namna hiyo), kuwa tu ni rafiki yako. Lakini wakati ninapojisikia kuongozwa kuja, kasha naweza kuja katika jina la Bwana Yesu. Ukitoa tu miguu yako kutoka katika ndege, yeye ni mali yako. Amina nalichukua hilo lote katika jina la Bwana Yesu. Kasha hauna kukutana naye nje pale, kwa sababu ni mabalozi wa Mungu (2korintho 5:18-20). Lakini sasa wakati kanisa Fulani, marafiki, hapa marafiki fulni, unaenda tu ukibahatisha tena, jamani kubahatisha nadhania mmechoka kusikiliza hilo.

Huna budi kuwa na Upako kukuongoza Ndugu. Na upako huo unakuja kwa Roho Mtakatifu, ndio, mkiongozwa na Roho, wana na Binti za Mungu wanaongozwa kwa Roho wa Mungu. Wanampenda Roho. Hawajaribu kusema, sasa, subiri dakika moja. Kanisa langu hawasemi "Amina" Kanisa langu hawainui kamwe mikono yao; wao ni kimya sana.
Wana wote na binti za Mungu wanaongozwa kwa Roho wa Mungu. Wanatembea kwa Roho wa Mungu. Wanatembea kwa Roho. Wakipekee, wakigeni, wanasimama kwa usahihi, na matendo yao yote ni sawa na Biblia.wanasimama, mafundisho yao yote husimama sawa na Biblia. Hawata pishana hata kwa jambo moja. Pale ambapo Biblia inasema hivyo, wanaendelea kwa hilo. Kama watasimama kwa dakika, wanajaribu kujifunza na kuona waende njia ipi. Na ndipo Roho Mtakatifu anapolifunua, na wanaendelea mbele. Na anafanya jambo lilelile, akifuata sheria zilezile, akiweka msingi uleule, Mungu tule yule anakuja juu yake na miujiza ileile, na maajabu yale yale na Ishara zile zile zinamfuata yeye ambazo zilimfuata yeye (Kristo)
Mungu atapokea kile ulicho toa, lakini anahitaji yote uliyo. Anahitaji kila kitu chako. Anahitaji yote. Anahitaji kila kitu ulicho nacho. Anahitaji maisha yako. Anahitaji shuhuda zako. Anahitaji kila dakika niishiyo anakutaka wewe uishi vema, utende vema unene vema, anataka kila kitu kisalimishwe kwake kwa uwaminifu.

*Kwamba* anaweza kukuongoza, na kukuelekeza, akuweke sehemu ambazo anataka wewe uende. Kuongozwa na Roho.

Shetani ni ndege mjanja na mwerevu. Anajua jinsi yakugonga jambo kabla hata halijaanza; anajua hilo. Unaona? Na jambo pekee unaloweza kufanya kumshinda ni kumtegemea Kristo na kujinyenyekeza mwenyewe na kumuachia yeye akuongoze. Kamwe hautalifanya kwa njia nyingine yoyote. Nguvu zako za kiakili kamwe hazitafanya. Unapaswa kuliamini hilo na umtumaini yeye. Yeye ni mchungaji si kazi ya kondoo kuwafukuza mbweha, ni kazi ya mchungaji; lakini kondoo lazima wakae na mchungaji ili wawe salama, hilo ni eneo langu la usalama. Ndani ya kristo na kristo ni neno. Hilo ndilo eneo la usalama. Roho Mtakatifu ndiye anatuongoza, sio seminary sio askofu na wanaona mbali, na kadhalika. Roho Mtakatifu ni kiongozi wetu.

Wangapi wana weza kukumbuka wakati Nabii mwema wa Mungu. Samweli wakati wa Waisraeli wote walipotaka kutenda kama watu wote wa ulimwengu! Je unalikumbuka hilo? Na Nabii akamwambia akisema, "Mnekosea" Lakini walitaka kutenda kama Wafilisti na kama wengine wote, vema, hilo ni kweli ndicho kilichotokea katika nyakati za kanisa la kwanza. Ni jambo la kigeni ambalo watu hawataki Mungu awaongoze, wanataka kufuata…… Wanataka mtu flani. Israel, walifanya kosa kubwa ambalo hawajawahi kufanya, wakati neema ilikuwa tayari imewapa Nabii, kiongozi, iliwatolea mwanakondoo kama Sadaka, iliwatolea chakula

kutoka mbinguni, na vitu vilivyo vizuri ambavyo Neema kua imewapatia; na bado katika (kutoka 15) walitaka sheria. Walitaka kufanya madaktari wa theolojia, na kuwa na mtu, walitaka kuwa na kitu flani kufanya zaidi. Mwanadamu siku zote anajaribu ku (kumkosea) ambaye amemuumba, na hafanyi lolote ila kujiua mwenyewe.

Lakini sasa watazame Israel, walikuwa wameona miujiza, hiyo ni ile Pentecoste ya mwanzoni; Israel, Wapentecoste wa siku hiyo. Sasa, walikuwa wametolewa kutoka Misri. Mungu alikuwa amewabariki, na kuwapa kila aina ya Ishara na maajabu, na kuwakomboa (kuwatoa) na wakati waliposimama juu ya baraka hiyo na walikula na makutano ya kipentecoste… Walifanya, sasa, sikiliza, Musa aliomba katika Roho, na Miriamu akatwaa zumari na kukimbia ukingoni, akipiga zumari, akicheza katika Roho, na binti wa Israeli wakamfuata, akicheza katika Roho. Na kama huo sio mkutano wa Kipentecoste, kamwe sijawahi kuona mmoja.

Hawakujua, hata kidogo ya kuwa nchi ya ahadi ilikuwa miaka 40 mbele yao. Lilikuwa miaka 40 tu. Lakini iliwachukuwa maika 40 kufika maili 40 ni kwa sababu walichagua kitu kisicho sahihi. Walichagua kuwa na sheria baada ya kumwacha Roho Mtakatifu awaongoze. Walitaka kuwa na kitu flani wangalitenda wenyewe; walitaka kuwa na kuhani flani, na watu wa sifa flani na theologia kidogo wangaliweza kubishania, badala yakuendelea nakumwacha Roho Mtakatifu awaongoze. Walikuwa katika Roho: Mungu aliwapa kila kitu; lakini walikuwa na kitu walitaka kufanya juu ya hilo.

Na mimi sio mnenaji mzuri, lakini na mpenda Bwana. Na siwezi kumpenda Kristo mpaka kwanza niwapende watu wake.hivyo kama nawapenda watu wake, kisha nampenda yeye na kisha nataka kuwa kama alivyo tenda. Nataka kuwa na kusudi sawa na kusudi alilokuwa nalo hilo lilikuwa siku zote nikijaribu kufanya (uzuri) kumsaidia mtu flani.

Sasa, kusema nina uongozi wa kwenda sehemu yoyote ya hizo, sina lakini najisikia kwamba ingepasa kupanda mbegu mahali flani kufanya vyovyote ningaliweza kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Nadhani Biblia inasema kwamba hatua za mwenye haki huimarishwa na Bwana (Zaburi 37:23). Sasa tunafanya vitu ambavyo si…… Hatuelewi kwnini tunafanya hivyo, lakini tunakaa tu. Ilimradi unaongozwa na Roho, nenda ulifanye kwa vyovyote. Inaweza iwe kinyume na mawazo yetu, lakini kama Roho Mtakatifu alisema, "Nenda" tunakwenda.

Kwa mfano sasa hivi, nina mkutano, unapaswa ufanyike New York, nitaufanya wiki hii, ambapo palikuwa na watu wapatao mia tatu wanaozungumza kihispania wanaenda kuichukuwa Bustani ya Square inayoingia watu kumi na tisa elfu wa kukaa, nao wanahitaji wiki hii hii ambayo niko hapa, ili niwe New York, Unaona? Lakini Roho Mtakatifu ameniongoza nije hapa (Port Alberni, Canada). Inaonekana kama ingekuwa kinyume. Lakini sijui kwa nini, lakini niko hapa unaona? Watoto wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu. Sisi hatuelewi.
Paulo alikuwa mfungwa wa Yesu Kristo, akitumika kwenye Neno lake kwa Roho ooh! Nalipenda hilo. Alikuwa amefungwa. Alikuwa amefungwa na mnyororo, na kongwa la upendo kufanya mapenzi ya Mungu na hayo tu. Alikuwa mfungwa alikuwa na kongwa la upendo. Alikuwa amefungwa kwa Kristo. Hawezi kufungwa na chochote kile.

Alifungwa na yeye, na popote alipoongozwa, hapo ndipo alipokuwa , bila kujali njia ilionekanaje kijani upande huu au ule. Ilibidi aende njia aliyoongozwa na kule kongwa lilikoenda.
Oh usiku wa leo, kama sisi kama Maskani ya Branham tungekuwa tu wafungwa kwa binafsi wa utu wetu wenyewe kwa matarajio yetu wenyewe kwamba tungeweza kujisalimisha kikamilifu wenyewe na kufungiwa kwake. Haijalishi dunia yote watafikiria nini, dunia yote inafanya nini, tumefungwa kwa kongwa la Upendo. Tu wafungwa. Mguu wangu umefungwa sana na Kristo, hauwezi kucheza dansi, macho yangu yamefungwa kwa Kristo mpaka….. Nionapo hawa waenda uchi wa mitaani, ninageuza kichwa changu; moyo wangu umefungwa katika Upendo na yeye mpaka sinao Upendo, Upendo na dunia hii tena. Mapenzi yangu yamefungwa sana kwake mpaka hata sijui yale nitakayo mimi ni nini. Ni popote anaponiongoza, nitamfuata, Bwana. Nitakuwa mfungwa (Waefeso 3:1 Waefeso 4:1 Filemoni 8:9)
Siamini kwamba mtumishi yoyote wa Mungu, anaeongozwa na roho, anaweza akaenda nje ya Mapenzi ya Mungu. Kwa sababu ili mradi anaongozwa na Roho. Hayo ni Mapenzi ya Mungu. Wakati mwingine unafanya mambo ambayo haelewi anavyofanya yeye mwenyewe na hajui kwa nini anafanya hilo lakini ni Mungu atendaye hilo kwa kutuletea mema "kila kitu kinatenda kazi kwa kuwapatia mema wale wampendao Mungu" (Rumi 8: 28).
Wapendwa wangu marafiki, nimejaribu maisha yangu yote, niwe chochote kile lakini nisiwe asiyesahihi. Nimejitehidi kuwa mwaminifu katika kushughulika kwangu na Mungu na wanadamu wenzangu. Na nimejaribu hilo wakati wote, kwenda na kutenda kama Roho Mtakatifu alivyo-niambia. Hiyo ndiyo sababu ninabebwa kutoka sehemu na kwenda sehemu, na kusimamisha mikutano, na kwenda sehemu sehemu kwa sababu nafuata uongozi wa Roho.

Nukuu za kingereza
Uongozi para 285.289.
Maisha yako yanaitoshea injili para 72-79.
Vitambulisho vitano para 1x4.
Paulo mfunwa wa Yesu Kristo uk 14-16.
Kushawishika na kuwajibika uk 7.
Mfalme aliekataliwa(---06-10) para 53.
Uhalisi usioshindwa wa Mungu (60-06-26) para 173-184.
Kutoka kwa tatu uku 33.
Nguvu za Mungu za kubadilisha para 177.
Wakati wa kanisa la simirna para 31-32-59-60.
Kuondoa shinikizo(62-05-13 jiono) para 28-29-16.
Mkuu kuliko Sulemani yuko hapa (62-07-25) para c-57.
Malkia wa sheba (60-07-10) para E-4.
Safina para 186.

Jiwe la kiroho la kujengea na 114 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schömberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306.
www.biblebelievers.de

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

Kwa nakala za kiingereza Kiswahili andika kwa
*Charles E. Kanju*
*Box 553 Korogwe – Tanga*
*Email: chaelika@live.com.*
*Cell phone: 0784 704299/ 0718230098*